JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2022

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2022

# 01 KISWAHILI

*Kimechapishwa na ;*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ........ 2

2.1 Sehemu A: Imla ........ 2
2.2 Sehemu B: Aina za Maneno ........ 7
2.3 Sehemu C: Nahau ........ 13
2.4 Sehemu D: Matumizi ya Alama za Uandishi ........ 16
2.5 Sehemu E: Ufahamu ........ 22

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ........ 28

4.0 HITIMISHO ........ 29

5.0 MAPENDEKEZO ........ 29

KIAMBATISHO CHA PEKEE ........ 31

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ya somo la Kiswahili katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2022. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa shule, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu sababu zilizochangia ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili. Vilevile, taarifa hii inaonesha jinsi ufundishaji na ujifunzaji ulivyomwezesha au kushindwa kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka minne.

Aidha, taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha. Baadhi ya sababu hizo ni kushindwa kutambua matakwa ya swali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu swali husika na athari ya lugha mama. Mtawanyiko wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi kwa kutumia vielelezo, chati na maelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa taarifa hii itawawezesha walimu na wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazosaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Kadhalika, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi, yatasaidia kuongeza umahiri wa wanafunzi na hatimaye kuimarisha ubora wa elimu nchini.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa mrejesho wa namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2022. Upimaji huu ulizingatia matakwa ya mtaala wa mwaka 2018 unaolenga kuimarisha umahiri wa mwanafunzi katika stadi za Kuzungumza, Kusikiliza, Kusoma na Kuandika.

Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na sehemu tano. Sehemu A ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno, sentensi, na kuyaandika (Imla). Sehemu B ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kubadili majina kuwa vitendo katika mawasiliano. Sehemu C ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutumia nahau na kuelewa maana zake katika lugha ya Kiswahili. Sehemu D ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kutumia alama za uandishi katika lugha ya Kiswahili. Sehemu E ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma na kuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi. Sehemu hizo zimetoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*. Kila sehemu ilikuwa na swali moja (1) lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama kumi (10).

Jumla ya wanafunzi 1,718,896 walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2022. Kati yao, wanafunzi 1,592,212 walifanya upimaji katika somo la Kiswahili ambapo wanafunzi 1,324,114 sawa na asilimia 83.19 walifaulu.

Viwango vya ufaulu katika majibu ya wanafunzi vimegawanyika katika sehemu nne kulingana na alama walizopata. Kiwango hafifu ni kati ya alama 0 - 2.5, kiwango cha wastani ni 3.0 - 6.0, kiwango kizuri 6.5 - 9.5 na kiwango kizuri sana ni alama 10.0. Wanafunzi waliopata wastani, kiwango kizuri na kizuri sana ndio waliohesabika kuwa wameweza

kujibu maswali kwa usahihi. Aidha, waliopata kiwango hafifu wameshindwa kujibu maswali kwa usahihi.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa wanafunzi katika kila swali umewasilishwa kwa njia ya chati. Rangi mbalimbali zimetumika kubainisha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi kwa kila swali ambapo rangi nyekundu imetumika kuwakilisha kiwango hafifu cha ufaulu, yaani asilimia 0 – 33, rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani, yaani asilimia 34 – 66 na rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri na kizuri sana yaani asilimia 67-100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inachambua majibu ya wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Aidha, idadi na asilimia ya wanafunzi waliojibu vizuri na walioshindwa kujibu vizuri imeoneshwa katika chati. Vilevile, taarifa hii imeonesha sababu za kufaulu na kutokufaulu kwa mwanafunzi katika kila swali. Sampuli za majibu ya wanafunzi zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu hafifu, wastani na mzuri katika maswali.

### 2.1 Sehemu A: Imla

Sehemu hii ilikuwa na swali moja ambalo lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali*. Wanafunzi walitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi tano (05) walizosomewa kwa sauti kisha kuziandika kwa usahihi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne yenye alama nusu ($00^{1}/_{2}$) kwa kila neno. Kila sentensi ilikuwa na alama 2; hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kuandika sentensi kwa kuzingatia kanuni za uandishi kama vile kuanza na herufi kubwa

mwanzoni mwa sentensi, alama ya nukta pamoja na kutambua sauti mbalimbali za matamshi ya silabi, maneno, na sentensi. Swali hilo ni:

**Swali la 1**: **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ______________________________________________

(ii) ______________________________________________

(iii) ______________________________________________

(iv) ______________________________________________

(v) ______________________________________________

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

(i) Mwaka ujao ukifika tutasherehekea.


(ii) Tumepata mafunzo ya mgambo.

(iii) Alijibanza pembeni ya nyumba.

(iv) Tutafanya usafi wa kinywa.

(v) Kitabu changu kipo maktaba.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,592,112 (100%) waliofanya upimaji. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,306,625 sawa na asilimia 82.1 walifaulu. **Chati Na. 1** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi hao kwa asilimia.





**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 496,895 (31.21%) walifanya vizuri sana kwani waliweza kuandika maneno yote ishirini kwa usahihi. Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika stadi ya kusikiliza na kuandika kwani waliweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano walizosomewa. Aidha, waliweza kubaini sauti zinazounda maneno yaliyosomwa na kuziandika kwa usahihi huku wakizingatia kanuni za uandishi kwa kutumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi na kuweka alama ya kituo mwishoni mwa sentensi.

Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na ujuzi wa kubaini na kuandika silabi zenye herufi mwambatano kama vile silabi ‘*‘mwa’’*, *“she”*, “*nzo”*, ‘‘*mbo’’*, ‘‘*nza’’, ‘‘mbe’’, ‘‘nyu’’, ‘‘mba’’, ‘‘nya*’’, ‘‘*nywa’’*, ‘‘*cha’’* na ‘‘*ngu’’* kwenye maneno kama vile “*mwaka*”, “*tutasherehekea*”, “*mafunzo*”, “*mgambo*”, “*alijibanza*”, “*pembeni*”, “*nyumba*”, “*tunafanya*”, “*kinywa*” na “*changu*” mtawalia. Maneno hayo ni miongoni mwa maneno yaliyounda sentensi tano za imla walizosomewa. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa

usahihi sentensi zote tano kwa kuzingatia kanuni za uandishi na hivyo kupata alama zote 10.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Mwaka ujao ukifika tutasherehekea.

(ii) Tumepata mafunzo ya mgambo.

(iii) Alijibanza pembeni ya nyumba.

(iv) Tunafanya usafi wa kinywa.


(v) Kitabu changu kipo maktaba.

Kielelezo Na. 1.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1*

Hata hivyo, wapo wanafunzi (43.93%) waliofanya vizuri lakini hawakuweza kupata alama zote 10 bali walipata kati ya alama 6.5 hadi 9.5 kutokana na kushindwa kuandika kwa usahihi baadhi ya maneno kuanzia 1 hadi 6. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza na kuandika kwa kuzingatia matamshi ya herufi zinazounda maneno pamoja na kanuni za uandishi ila walishindwa kuandika kwa usahihi maneno yote.

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 110,333 sawa na asilimia 6.93 walipata alama za wastani. Wanafunzi hao waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 12 kati ya maneno 20 ya sentensi zote tano. Wanafunzi hao, walishindwa kuandika baadhi ya maneno yenye silabi za herufi mwambatano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja badala ya kuandika neno ‘‘tutasherehekea’’ aliandika ‘‘*tutashetalekea”,* ‘‘mafunzo’’ aliandika ‘‘*mafuzwo*’’ ‘‘mgambo’’ aliandika ‘‘*mngambo*’’. Pia, katika neno ‘‘Tutafanya’’ aliandika ‘‘tunafamyu’’ na neno “kinywa” aliandika ‘‘*kimlwa*’’ na sentensi ya tano neno ‘‘kipo’’ aliandika ‘‘*kimpo*’’ na neno ‘‘maktaba’’ aliandika

“*makitaba”*. Vilevile, mwanafunzi huyo alishindwa kuzingatia alama za uandishi kwani alianza na herufi ndogo badala ya herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi baadhi ya maneno na kupata alama za wastani.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) mwaka uja ukifika tutashelekea.

(ii) tumepata mafuria ya mgamba.

(iii) aliji bcria pembe ya nyumba.

(iv) tunafanya usafi wakinya .


(v) kitabu chagu kipo makitamba.

Kielelezo Na. 1.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 1*

Kielelezo Na.1.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi maneno saba kati ya ishirini na hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 285,487 sawa na asilimia 17.93 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa sababu walishindwa kuandika kwa usahihi maneno waliyosomewa. Baadhi yao waliandika maneno bila kuzingatia kanuni za uandishi ambapo walichanganya herufi kubwa na ndogo. Wengine hawakuacha nafasi kati ya neno moja na neno lingine huku wengine walitenganisha silabi za neno moja na silabi nyingine katika kuunda neno. Pia wengine walianza na herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi na pia hawakuweka alama ya kituo mwishoni mwa sentensi. Vilevile, wanafunzi wengine katika kundi hili hawakuelewa matakwa ya swali kwani walinakili maelekezo yaliyopo kwenye karatasi ya upimaji na kujaza sehemu iliyoachwa wazi badala ya kuandika sentensi walizosomewa. Zaidi ya hayo, wanafunzi wengine katika

kundi hili waliandika miandiko isiyosomeka kutokana na kutokumudu stadi za Kusikiliza na Kuandika. Kielelezo Na. 1.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika kwa usahihi maneno mengi aliyosomewa.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) mwaka ujo ukikia tuta sekeA

(ii) bamepaba mazo nga ~~ngo~~ ya mka

(iii) Alijiba za papeni ya Ronba

(iv) tanafanga usifi wa kiwoma

(v) kitaba changa kupo makitaba

Kielelezo Na. 1.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1*

Kielelezo Na. 1.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye aliandika kinyume na matakwa ya swali isipokuwa neno *mwaka* katika kipengele cha (i) aliandika kwa usahihi.

## 2.2 Sehemu B: Aina za Maneno

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano. Kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2) na kufanya swali kuwa na jumla ya alama kumi (10). Swali lilimpima mwanafunzi kuhusu dhana ya aina za maneno na lilimtaka kubadili majina kuwa vitendo. Swali hilo ni:

**Swali la 2** Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Somo ________(Msomaji, Soma, Msomi).


(ii) Mchezo ________(Michezo, Mchezaji, Cheza).

(iii) Mwandiko _______(Andika, Andiko, Mwandishi).

(iv) Kipimo _________(Vipimo, Pima, Mpimaji).

(v) Mwaliko _________(Mwalikwa, Mwalikaji, Alika).

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma* ambapo lilimtaka mwanafunzi kubadili majina kuwa vitendo. Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,592,112 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa sababu wanafunzi 757,250 sawa na asilimia 47.56 ndio waliofaulu. **Chati Na. 2** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi hao.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 388,682 sawa na asilimia 24.42 waliweza kubaini vitenzi vilivyotokana na majina waliyopewa. Miongoni mwao, wanafunzi 288,586 sawa na asilimia 18.13 walifanya vizuri sana na kupata alama zote 10. Kwa mfano, wanafunzi hao walibadili katika kipengele cha (i) jina *Somo* kuwa *Soma*, (ii) jina *Mchezo* kuwa *Cheza,* (iii) jina *Mwandiko* kuwa *Andika,* (iv) jina *Kipimo* kuwa *Pima* na (v) jina *Mwaliko* kuwa *Alika*. Hata hivyo, wapo wanafunzi waliofanya vizuri swali hili na kupata alama za juu kwa kuandika kwa usahihi vipengele vinne na kushindwa kuandika kwa usahihi kipengele kimoja na hivyo kupata alama 8. Hii inaonesha kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za

maneno. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na umahiri wa kubadili majina kuwa vitendo.

2. Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Somo ___Soma___ (Msomaji, Soma, Msomi).

(ii) Mchezo ___Cheza___ (Michezo, Mchezaji, Cheza).

(iii) Mwandiko ___Andika___ (Andika, Andiko, Mwandishi).


(iv) Kipimo ___Pima___ (Vipimo, Pima, Mpimaji).

(v) Mwaliko ___Alika___ (Mwalikwa, Mwalikaji, Alika).

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2*

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubadili kwa usahihi majina kuwa vitendo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye maneno aliyopewa katika mabano kwa kila kipengele.

Aidha, wanafunzi 368,568 sawa na asilimia 23.15 walipata alama za wastani kwa kuwa wanafunzi hao waliweza kubadili baadhi ya majina kuwa vitendo na kushindwa kubadili majina mengine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibadili kwa usahihi jina "*Somo*" kuwa '*Soma'* katika kipengele (i), "*Mchezo*" kuwa '*cheza*' katika kipengele cha (ii) "*Mwandiko*" kuwa '*Andika*' katika kipengele (iii) lakini katika kipengele cha (iv) alibadili jina "*kipimo*" kuwa "*Vipimo"* badala ya ''*pima*''. Aidha, katika kipengele cha (v) alibadili jina "*Mwaliko*" kuwa "*mwalikwa"* badala ya ''*Alika''.* Uandishi wa majibu hayo unaonesha kuwa wanafunzi katika kundi hili hawakuwa na umahiri wa kutosha wa aina za maneno, kwani walishindwa kubaini kuwa neno "vipimo" na "mwaliko" ni nomino na si vitendo kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.2 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliopata alama za wastani.



2. Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Somo Soma (Msomaji, Soma, Msomi).

(ii) Mchezo Michezo (Michezo, Mchezaji, Cheza).


(iii) Mwandiko Andika (Andika, Andiko, Mwandishi).

(iv) Kipimo Pima (Vipimo, Pima, Mpimaji).

(v) Mwaliko Mwalikaji (Mwalikwa, Mwalikaji, Alika).

Kielelezo Na. 2.2 (a): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani*

Katika kielelezo Na. 2.2 (a) mwanafunzi aliweza kubadili majina kuwa vitendo katika kipengele cha (i), (iii) na (iv) lakini katika kipengele cha (ii) neno "*michezo*" sio kitendo bali ni wingi wa neno "Mchezo" na kitendo chake ni "cheza". Katika kipengele cha (v) neno "*mwalikaji*" sio kitendo cha jina "*mwaliko*" bali ni mtu anayewakaribisha watu kuhudhuria hafla fulani na kitendo chake ni "Alika".



2. Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Somo ngoma (Msomaji, Soma, Msomi).

(ii) Mchezo michezo (Michezo, Mchezaji, Cheza).

(iii) Mwandiko Andiko (Andika, Andiko, Mwandishi).

(iv) Kipimo Pima (Vipimo, Pima, Mpimaji).

(v) Mwaliko aika (Mwalikwa, Mwalikaji, Alika).

Kielelezo Na. 2.2 (b): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani*

Kielelezo Na. 2.2 (b) kinaonesha mwanafunzi aliyeweza kubadili majina kuwa vitendo katika kipengele cha (iii) na (iv), na alishindwa kubadili katika kipengele cha (i), (ii) na (v). Mwanafunzi huyo aliandika

neno “ngoma” katika kipengele cha (i) na “aika” katika kipengele cha (v) maneno ambayo hayakuwepo kwenye machaguo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 514,210 sawa na asilimia 32.30 walishindwa kubadili majina waliyopewa katika vipengele vyote vitano kuwa vitendo kwa kuchagua maneno yasiyo sahihi kati ya maneno waliyopewa kwenye mabano. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kubadili majina kuwa vitendo. Kwa mfano, mwanafunzi mmojawapo katika kipengele cha (i) alibadili jina ‘‘*Somo*’’ kuwa kitendo kwa kuandika ‘‘*cheza’’* ambalo si kitendo cha jina “*somo*” bali ni kitendo cha jina “*mchezo*”, kipengele cha (ii) jina “*Mchezo*” lilibadilishwa na kuwa kitendo *“Andiko”* kipengele cha (iii) jina “*Mwandiko*” lilibadilishwa na kuwa kitendo *“mwandishi*” na kipengele cha (iv) jina “*Kipimo*” lilibadilishwa na kuwa kitendo “*mpimaji*”*.* Maneno yaliyobainishwa na mwanafunzi huyo ni majina na si vitendo vya majina aliyopewa. Aidha, katika kipengele cha (v) jina “*Mwaliko*” lilibadilshwa na kuwa kitendo *“alikamsomi”* ambayo ni maneno yaliyokuwepo kwenye orodha ya maneno ya kuchagua katika mabano ambapo mwanafunzi huyo aliyaandika bila kuweka nafasi. Hata hivyo, jibu hilo halikuwa sahihi kutokana na kuleta maana tofauti iliyosababishwa na kuunganisha neno “*alika”* na “*msomi*”. Kwa upande mwingine, wanafunzi 320,652 sawa na asilimia 20.14 waliweza kubadili jina kuwa kitendo katika kipengele kimoja na kupata alama 2. Kielelezo Na. 2.3 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali kwa usahihi.

2. Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Somo ___msomaji___ (Msomaji, Soma, Msomi).

(ii) Mchezo ___Mchezaji___ (Michezo, Mchezaji, Cheza).

(iii) Mwandiko ___mwandishi___ (Andika, Andiko, Mwandishi).

(iv) Kipimo ___Mpimaji___ (Vipimo, Pima, Mpimaji).

(v) Mwaliko ___mwalikwa___ (Mwalikwa, Mwalikaji, Alika).

Kielelezo Na. 2.3 (a): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2*

Majibu katika kielelezo Na. 2.3 (a) yanaonesha kuwa, mwanafunzi hakuelewa matakwa ya swali kwani alichagua maneno ya mtenda badala ya vitendo katika vipengele vyote. Hii inaonesha kuwa mwanafunzi huyo alishindwa kutofautisha majina na vitendo.

2. Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Somo ___kiswahili___ (Msomaji, Soma, Msomi).

(ii) Mchezo ___Kuchezi___ (Michezo, Mchezaji, Cheza).

(iii) Mwandiko ___simuandishi___ (Andika, Andiko, Mwandishi).

(iv) Kipimo ___simupimaji___ (Vipimo, Pima, Mpimaji).

(v) Mwaliko ___usilalike___ (Mwalikwa, Mwalikaji, Alika).

Kielelezo Na. 2.3 (b): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama hafifu swali la 2*

Kielelezo Na. 2.3 (b) kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambayo hayana uhusiano na matakwa ya swali kwani maneno aliyoandika katika kila kipengele hayakupendekezwa katika maneno aliyopewa kwenye mabano.

## 2.3 Sehemu C: Nahau

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) na lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana Katika Miktadha Mbalimbali*. Swali lilipima matumizi ya nahau na maana zake. Jumla ya alama katika swali hili ilikuwa 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 02. Swali hilo ni:

**Swali la 3:** Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maana ya nahau zifuatazo:

(i) Pata jiko___________________________________


(ii) Shingo upande _____________________________

(iii) Ndimi mbili_________________________________

(iv) Vaa miwani ________________________________


(v) Zunguka mbuyu _____________________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,592,112 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu kilikuwa cha wastani ambapo wanafunzi 606,363 sawa na asilimia 38.08 waliweza kujibu vizuri. Aidha, wanafunzi 985,749 sawa na asilimia 61.92 walipata alama za kiwango hafifu. **Chati Na. 3** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 3**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

Chati Na.3 inaonesha kuwa, wanafunzi 27,227 sawa na asilimia 1.71 walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu. Wanafunzi hao waliweza kuandika maana sahihi ya kila nahau waliyopewa katika vipengele vyote. Majibu yao yalionesha kuwa, wana uelewa wa kutosha juu ya nahau walizopewa na maana zake. Kwa mfano, katika kipengele (i) *Pata jiko* (ii) *Shingo upande* (iii) *Ndimi mbili* (iv) *Vaa miwani* (v) *Zunguka mbuyu* waliandika (i) *Kuoa* (ii) *Kukubali jambo pasipo hiari ya moyo/kupenda* (iii) *Kigeugeu* (iv) *Kulewa pombe* na (v) *Kutoa/Kupokea/Kula rushwa* mtawalia. Wanafunzi 70,891 sawa na asilimia 4.45 waliandika kwa usahihi maana za nahau nne na kushindwa nahau moja; hivyo kupata alama 8. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote vya swali kwa usahihi.


3. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maana ya nahau zifuatazo:

(i) Pata jiko kuoa

(ii) Shingo upande kukubali bila kupenda

(iii) Ndimi mbili kigeugeu


(iv) Vaa miwani kulewa pombe

(v) Zunguka mbuyu kutoa rushwa

Kielelezo Na. 3.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 508,245 sawa na asilimia 31.92 walipata alama za wastani kwani waliweza kuandika maana sahihi za nahau katika vipengele 2 au 3 na kushindwa katika vipengele vingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele cha (i) aliandika maana ya nahau *Pata jiko* kuwa ni *kuoa*. Kipengele cha (iv) *Vaa miwani* aliandika kuwa ni *kulewa pombe* na kipengele cha (v) *Zunguka mbuyu* aliandika kuwa ni *Kutoa rushwa* maana ambazo zilikuwa sahihi. Hata hivyo, katika kipengele (ii) aliandika maana ya

nahau *Shingo upande kuwa* ni *Kuona* wivu badala ya *kukubali jambo pasipo hiari ya moyoni* na kipengele cha (iii) *Ndimi mbili* aliandika kuwa ni *kinyanga* badala ya *kigeugeu/kukosa msimamo*. Maana katika vipengele (ii) na (iii) zinaonesha kuwa mwanafunzi huyo hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana ya nahau husika. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.


3. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maana ya nahau zifuatazo:
(i) Pata jiko Kuoa
(ii) Shingo upande sikitika
(iii) Ndimi mbili Mto
(iv) Vaa miwani Kulewa pombe
(v) Zunguka mbuyu mkanda

Kielelezo Na. 3.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 3*

Kielelezo Na. 3.2, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuandika maana sahihi kama vile; "*kuoa*" katika kipengele cha (i) na kipengele cha (iv) "*kulewa pombe*". Mwanafunzi huyo alionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya nahau kuwa hutumia lugha ya picha ili kueleza au kuficha jambo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 985,749 (61.92%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walipata kupata alama kuanzia 0 hadi 2.0. Wanafunzi hao walikosa umahiri kuhusu matumizi na maana ya nahau katika miktadha mbalimbali; hivyo walitoa maana zisizo sahihi na kushindwa kukidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika maana zisizo sahihi za nahau alizopewa katika vipengele vyote vitano kama vile; (i) *pata mchumba*, (ii) *kukuba kishingo upande*, (iii) *ndege*, (iv) *kuzima macho* na kipengele cha (v) *kujificha*. Maana ambazo hazikuakisi maana ya nahau (i) Pata jiko, (ii)

Shingo upande, (iii) Ndimi mbili, (iv) Vaa miwani na (v) Zunguka mbuyu mtawalia. Kielelezo Na. 3.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

3. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maana ya nahau zifuatazo:
   (i) Pata jiko ___Pata___
   (ii) Shingo upande ___Shingo___
   (iii) Ndimi mbili ___upande___
   (iv) Vaa miwani ___Ndimi mbili___
   (v) Zunguka mbuyu ___Vaa miwani___

Kielelezo Na. 3.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3*

Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyenakili baadhi ya maneno kutoka kwenye nahau alizopewa badala ya kuandika maana ya nahau husika.

## 2.4 Sehemu D: Matumizi ya Alama za Uandishi

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kilikuwa na nafasi mbili zilizo wazi. Mwanafunzi alitakiwa kujaza alama sahihi za uandishi katika nafasi hizo. Kila nafasi ilikuwa na alama 1 na kufanya kila kipengele kuwa na alama 2. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10. Umahiri mkuu uliopimwa ulikuwa ni *Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* kwa kutumia alama za uandishi. Swali hilo ni:

**Swali la 4:** Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Alaa ___ Mambo gani haya____


(ii) Je __ huyu ni mtoto wako ___

(iii) Hekoo ___ timu yetu imepata ushindi ___

(iv) Wanafunzi waliandaa nyimbo ___ mashairi na ngonjera ___

(v) Haa ___ kumbe____

Wanafunzi waliolijibu swali hili walikuwa 1,592,112 sawa na asilimia 100. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo wanafunzi 562,771 sawa na asilimia 35.34 walipata alama 4.0 hadi 10.0. Aidha, wanafunzi 1,029,341 sawa na asilimia 64.66 walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 0 hadi 3.0 kama inavyoonekana katika **Chati Na. 4**.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Wanafunzi wachache 6,730 sawa na asilimia 0.42 walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani walijibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Wanafunzi hao walionesha umahiri mkubwa katika matumizi ya alama za uandishi kwa kukidhi matakwa yote ya swali. Wanafunzi hawa, waliweza kuweka alama sahihi za uandishi katika nafasi zilizoachwa wazi; hivyo kufanya sentensi nzima kuwa na mtiririko unaoleta maana. Wanafunzi hao walielewa kuwa alama ya mshangao (**!**) inawekwa kwenye maelezo ya kushangaza na alama ya kuuliza (**?**) inawekwa kwenye maelezo au sentensi zinazouliza maswali

na mara nyingi huwekwa mwishoni mwa sentensi. Pia, waliweza kubaini kuwa alama ya mkato (**,**) hutumika kuonesha pumziko dogo katika sentensi na kutenganisha vitu vilivyoorodheshwa na alama ya nukta au kituo kikubwa (**.**) huwekwa mwishoni mwa sentensi. Hata hivyo, baadhi yao waliandika kwa usahihi alama za uandishi katika vipengele vitatu au vinne kati ya vitano walivyopewa. Kwa ujumla, wanafunzi hawa walikuwa na umahiri mkubwa uliowawezesha kubaini alama sahihi za uandishi zilizohitajika katika sentensi walizopewa. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Alaa ! Mambo gani haya ?

(ii) Je , huyu ni mtoto wako ?

(iii) Hekoo ! timu yetu imepata ushindi .


(iv) Wanafunzi waliandaa nyimbo , mashairi na ngonjera .

(v) Haa ! Kumbe !

Kielelezo Na. 4.1**:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4

Aidha, wanafunzi 335,311 sawa na asilimia 21.06 walipata alama za wastani kuanzia 4.0 hadi 6.0 kwani waliweza kuandika kwa usahihi alama za uandishi katika nafasi nne hadi sita kati ya kumi zilizoachwa wazi. Hii ilitokana na wanafunzi hao kushindwa kutofautisha matumizi sahihi ya baadhi ya alama za uandishi. Baadhi ya wanafunzi walishindwa kutofautisha alama ya mkato (,) na kituo kikubwa au nukta (.) hasa katika mazingira ya utokeaji na matumizi yake katika sentensi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele cha (i) sehemu ya kwanza aliandika irabu (**i**) badala ya alama ya mshangao (**!**). Katika

kipengele cha (ii) sehemu ya kwanza aliandika alama ya kuuliza (**?**) badala ya alama ya mkato au kituo kidogo (**,**). Kipengele cha (iii) sehemu ya kwanza aliandika alama ya kuuliza (**?**) badala ya alama ya mshangao (**!**). Kipengele cha (iv) sehemu ya kwanza aliweka kituo kikubwa (**.**) badala ya mkato au kituo kidogo (**,**) na kipengele cha (v) sehemu zote mbili aliweka kituo kikubwa (**.**) badala ya alama ya mshangao (**!**). Hata hivyo, mwanafunzi huyo aliandika kwa usahihi alama za uandishi katika kipengele (i), (ii), (iii) na (iv) sehemu ya pili hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo Na. 4.2 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliopata alama za wastani.



4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Alaa « » Mambo gani haya ?

(ii) Je ? huyu ni mtoto wako .


(iii) Hekoo ? timu yetu imepata ushindi .

(iv) Wanafunzi waliandaa nyimbo . mashairi na ngonjera ?

(v) Haa . Kumbe .

Kielelezo Na. 4.2 (a): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani swali la 4*

Kielelezo 4.2 (a) ni majibu ya mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi alama za uandishi katika kipengele cha (i) sehemu ya pili, kipengele cha (ii) sehemu ya kwanza, kipengele cha (iii) sehemu zote mbili na kipengele cha (v) sehemu ya kwanza. Aidha, alishindwa kuandika kwa usahihi alama za uandishi katika kipengele cha (i) sehemu ya kwanza, kipengele cha (ii) sehemu ya pili, kipengele cha (iv) sehemu zote mbili na kipengele cha (v) sehemu ya pili.


4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Alaa_____ Mambo gani haya__!___

(ii) Je__?___ huyu ni mtoto wako__?___

(iii) Hekoo__!__ timu yetu imepata ushindi__!___

(iv) Wanafunzi waliandaa nyimbo__]___ mashairi na ngonjera__!___


(v) Haa__!___ Kumbe__!___

Kielelezo Na. 4.2 (b): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani swali la 4*

Kielelezo Na. 4.2 (b) kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi alama za uandishi katika kipengele cha (i) sehemu ya kwanza, kipengele cha (ii) sehemu ya pili, kipengele cha (iii) sehemu ya kwanza na kipengele cha (v) sehemu zote mbili. Hata hivyo, alishindwa kuandika kwa usahihi alama za uandishi katika kipengele cha (i) sehemu ya pili, kipengele cha (ii) sehemu ya kwanza, kipengele cha (iii) sehemu ya pili na kipengele cha (iv) sehemu zote mbili.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 1,029,341 sawa na asilimia 64.66% walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walipata alama kuanzia 0 hadi 3.0. Wanafunzi hao walishindwa au waliweza kuandika alama sahihi za uandishi katika nafasi moja hadi tatu kati ya kumi zilizoachwa wazi. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya matumizi ya alama mbalimbali za uandishi katika sentensi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika herufi A na B, B na A, C na D, A na D na D na A katika vipengele (i), (ii), (iii), (iv) na (v) kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 4.3: (a) na (b) kinaonesha sampuli ya majibu ya

wanafunzi walioshindwa kuweka alama sahihi za uandishi katika sentensi walizopewa na kupata alama hafifu.


4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Alaa__?__ Mambo gani haya__((__

(ii) Je__.__ huyu ni mtoto wako__!__


(iii) Hekoo__((__ timu yetu imepata ushindi__!__

(iv) Wanafunzi waliandaa nyimbo__.__ mashairi na ngonjera__?__

(v) Haa__))__ Kumbe__?__

Kielelezo Na. 4.3 (a): *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 4*

Kielelezo Na. 4.3 (a) kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweka alama za uandishi zisizo sahihi kwenye nafasi zilizoachwa wazi kwa kuweka alama zifuatazo. Kipengele (i) aliweka alama ya kuuliza *"?"* badala ya mshangao *"!"* sehemu ya kwanza na sehemu ya pili aliweka alama "((" badala ya alama ya kuuliza *"?"*, kipengele cha (ii) sehemu ya kwanza aliweka nukta *"."* badala ya mkato *","* na sehemu ya pili aliweka alama ya mshangao *"!"* badala ya alama ya kuuliza *"?"*, kipengele cha (iii) aliweka alama *"(("* na *"!"* badala ya alama *"!"* na *"."*, kipengele (iv) aliweka alama *"."* na *"?"* badala ya *","* na *"."* na kipengele cha (v) aliweka alama *"))"* na *"?"* badala ya alama *"!"* na *"!"*.



4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Alaa ma Mambo gani haya Jamani

(ii) Je wangu huyu ni mtoto wako nwangani

(iii) Hekoo a timu yetu imepata ushindi Simba

(iv) Wanafunzi waliandaa nyimbo nzuri mashairi na ngonjera vizuri

(v) Haa sang Kumbe Sawa

Kielelezo Na. 4.3 (b): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi lisilo sahihi katika swali la 4*

Kielelezo Na. 4.3 (b) kinaonesha mwanafunzi hakuelewa matakwa ya swali. Mwanafunzi huyo aliandika maneno katika sehemu zilizoachwa wazi badala ya kuandika alama za uandishi.

## 2.5 Sehemu E: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kusoma hadithi, kuielewa na kujibu maswali.

**Swali la 5:** Soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

*Jina langu ni Imani. Ninasoma Darasa la nne. Siku moja nilitumwa kwa bibi kuleta jagi la maziwa. Kulikuwa na giza totoro. Wakati wa kurudi nyumbani nilipita karibu na dimbwi la maji. Nilisikia sauti, ''Nywaa! Nywa! Nywa!'' Kila nikijaribu kujificha nilisikia sauti hizo zikirudia, ''Nywa!'' Nilidhani ninaambiwa ninywe maziwa yote.*

*Nilipofika nyumbani niliwaambia wazazi wangu kuwa kuna sauti za kutisha kutoka kwenye dimbwi ambazo ziliniamuru ninywe maziwa yote. Dada yangu Tumaini alicheka sana akasema, ‘‘Hizo ni sauti za chura.’’ Pia, wazazi wangu walicheka na kuniambia nisiwe mwoga.*

**Maswali**

(i) Je, Imani alitumwa kwa Bibi kuleta nini?

________________________________________

(ii) Nini maana ya nahau ‘‘giza totoro’’ kama ilivyotumika katika habari uliyosoma?

________________________________________

(iii) Imani alipokuwa anarudi nyumbani alisikia nini?

________________________________________


(iv) Je, kwa nini Tumaini alicheka?

________________________________________

(v) Habari hii inatufundisha nini?

________________________________________

Jumla ya wanafunzi 1,592,112 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani wanafunzi 1,005,737 sawa na asilimia 63.17 walifaulu. Aidha, wanafunzi 586,375 sawa na asilimia 36.83 walikuwa na ufaulu hafifu ambapo walikuwa na alama kuanzia 0 hadi 2.5. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili umeoneshwa katika **Chati Na. 5**.




**Chati Na. 5**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa wanafunzi 383,139 sawa na asilimia 24.1 walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Miongoni mwao, wanafunzi 98,869 sawa na asilimia 6.21 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10.0. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana, miongoni mwao (209,579 (13.2%) walipata alama 8.0. Hii ni kutokana na wanafunzi hao kujibu kwa usahihi vipengele vinne kati ya vitano. Kwa ujumla majibu yao yanaonesha kuwa wanafunzi hawa walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma habari na kuelewa maudhui yaliyomo kwenye habari husika. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi na kukidhi matakwa ya swali katika kila kipengele.

**Maswali**:

(i) Je, Imani alitumwa kwa Bibi kuleta nini?

Kuleta jagi la maziwa

(ii) Nini maana ya nahau "giza totoro" kama ilivyotumika katika habari uliyoisoma?

Giza nene

(iii) Imani alipokuwa anarudi nyumbani alisikia nini?

Alisikia sauti ya nywaa! nywaa! nywaa!

(iv) Je, kwa nini Tumaini alicheka?

Alicheka baada yakujua mdogo wake aliogopa sauti ya chura

(v) Habari hii inatufundisha nini?


Tusiwe waoga

Kielelezo Na. 5.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5*

Kielelezo Na. 5.1, ni majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri vipengele vyote 5 kwa kuwa alikuwa na umahiri wa kusoma hadithi na kuelewa maudhui.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 622,598 sawa na asilimia 39.11 walipata alama za wastani kuanzia 3.0 hadi 6.0 kutokana na kuwa na umahiri wa wastani katika kusoma na kubaini maudhui yaliyomo kwenye habari husika. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (ii) kilichomtaka kutoa maana ya *giza totoro* kama ilivyotumika katika habari aliyosoma badala yake alitoa maana kwa kuandika *wakati wa kurudi nyumbani* maneno aliyonakili kutoka katika habari aliyosoma. Kipengele cha (v) alieleza kuwa habari inatufundisha *tusiwe tunatembea usiku* jambo ambalo sio funzo linalotolewa na habari aliyosoma lakini aliweza kuandika majibu sahihi kama vile, katika kipengele cha (i) *Jagi la*

*maziwa*, (iii) *Sauti ikisema Nywaa, Nywaa, Nywaa* na kipengele cha (iv) *kwa sababu ilikuwa ni sauti ya chura*. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele kwa usahihi na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine na kupata alama za wastani.


**Maswali**:

(i) Je, Imani alitumwa kwa Bibi kuleta nini?

Jagi la maziwa

(ii) Nini maana ya nahau "giza totoro" kama ilivyotumika katika habari uliyoisoma?

Alipita Kalibu na ndimbwi

(iii) Imani alipokuwa anarudi nyumbani alisikia nini?

Alisikia Sauti Nywaa Nywaa Nywaa

(iv) Je, kwa nini Tumaini alicheka?

Hizo ni Sauti za chara

(v) Habari hii inatufundisha nini?


Kutumwa na wazazi wako ukubari

Kielelezo Na. 5.2: *Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 5*

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuandika majibu sahihi katika kipengele cha (i) na cha (iii).

Aidha, wanafunzi 586,375 sawa na asilimia 36.83 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma habari na kuelewa maudhui yaliyomo na wengine walishindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu vibaya swali na kupata alama 0 kwani alinakili maneno yaliyokuwa kwenye habari aliyosoma kama vile,

kipengele cha (i) *zikirudia,* kipengele cha (ii) *kila nikijaribu kuficha nilishikia sauti hizo zikirudia* ambapo neno *nilishikia* lilipaswa kuwa *nilisikia*. Pia, kipengele cha (iii) alinakili maneno *nilipita karibu na dimbwi la maji nilisikia sauti*, kipengele cha (iv) *kuleta jai maziwa kulikuwa iza totoro* na kipengele cha (v) *nilisikia sauti* badala ya kujibu maswali kutokana na habari aliyosoma. Vilevile, mwanafunzi huyu aliandika neno *jai* badala ya *jagi* na *iza* badala ya *giza*. Wengine walijibu kwa kunakili maneno ya kutoka kwenye nahau *giza totoro*. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika kama ifuatavyo: kipengele cha (i) *giza* na kipengele cha (iii) *totoro*. Kielelezo Na. 5.3 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali kwa usahihi.



**Maswali**:

(i) Je, Imani alitumwa kwa Bibi kuleta nini?

Kumasaldia muzehe

(ii) Nini maana ya nahau "giza totoro" kama ilivyotumika katika habari uliyoisoma?

danasara nne

(iii) Imani alipokuwa anarudi nyumbani alisikia nini?

Aricheka Kuniambia kuambiyansemwo

(iv) Je, kwa nini Tumaini alicheka?

maziwa wacheka

(v) Habari hii inatufundisha nini?

Kukukukuwa na kulikuwa nangae

Kielelezo Na. 5.3 (a): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika katika swali la 5*

Katika kielelezo Na. 5.3 (a) mwanafunzi ameandika majibu yasiyoshabihiana na habari aliyoisoma jambo linaloonesha kuwa hana umahiri wa kusoma habari na kuelewa maudhui.

**Maswali**:

(i) Je, Imani alitumwa kwa Bibi kuleta nini?

Kuleta jongi la maziwa kulikuwana giza totoro

(ii) Nini maana ya nahau "giza totoro" kama ilivyotumika katika habari uliyoisoma?

n giza la maziwa ya totoro

(iii) Imani alipokuwa anarudi nyumbani alisikia nini?

alisikia sauti ya nyao, nyao,

(iv) Je, kwa nini Tumaini alicheka?

nina ambiwa ni nywe maziwa nilikunya maziwa yote

(v) Habari hii inatufundisha nini?

Habali hii Inatufundisha kusoma

Kielelezo Na. 5.3 (b): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5*

Kielelezo Na. 5.3 (b) kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye alikosa umahiri wa kusoma na kuelewa habari na kuandika majibu yasiyokidhi matakwa ya swali kwenye kila kipengele.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali na Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma*. Upimaji huu ulikuwa na maswali matano ambayo yalipima uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza na kuandika sauti mbalimbali za matamshi ya maneno na sentensi (Imla), umahiri wa aina za maneno, kutoa maana ya nahau, umahiri wa kutumia alama sahihi za uandishi katika sentensi pia kusoma na kujibu maswali yatokanayo na habari.

Uchambuzi unaonesha kuwa, umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* ulipimwa katika swali la 1, 3 na 4 na ulikuwa na ufaulu wa

wastani wa asilimia 51.84. Aidha, umahiri wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma* ulipimwa katika swali la 2 na 5. Umahiri huo ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 55.38. Taarifa za uchambuzi huu zimeambatanishwa kwenye **Kiambatisho cha Pekee**.

## 4.0 HITIMISHO

Ufaulu wa jumla wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili 2022 ni mzuri sana kwani wanafunzi 1,324,114 sawa na asilimia 83.19 walifaulu katika upimaji huo kwa kupata alama 10 hadi 50. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kusikiliza na kuandika sauti mbalimbali za matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), kutambua aina za maneno, kutoa maana ya nahau, kuandika alama sahihi za uandishi pamoja na kusoma, kuelewa na kujibu maswali yatokanayo na habari waliyosoma.

Aidha, jumla ya wanafunzi 267,998 sawa na asilimia 16.81 walikuwa na ufaulu hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kujibu maswali kwa ufasaha kutokana na changamoto mbalimbali kama vile: kutokumudu stadi za Kusoma na Kuandika kwani walishindwa kujibu kwa ufasaha maswali yatokanayo na habari waliyopewa, athari ya lugha mama, kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa umahiri wa kutoa maana za nahau walizopewa, kukosa umahiri wa matumizi sahihi ya alama za uandishi katika sentensi pamoja na kushindwa kubadili majina kuwa vitendo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Pamoja na ufaulu mzuri sana wa somo la Kiswahili hatua za makusudi hazina budi kuchukuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa miaka ijayo. Hatua hizo ni kama ifuatavyo*:*

(a) Walimu wawapatie wanafunzi mazoezi ya kutosha ya kutumia maneno yenye herufi mwambatano kama vile; *mw, nz, mb, ny, nyw, ch, ng*. Hii itawawezesha wanafunzi kumudu kutamka na kuandika maneno yanayoundwa na herufi hizo.

(b) Walimu watumie kadi za manila au chati ili kuwawezesha wanafunzi kubaini maumbo ya majina yanayobadilika kuwa vitendo. Hii itawezesha wanafunzi kuwa na umahiri wa kubadili majina kuwa vitendo, hivyo kukuza mawasiliano yao.

(c) Walimu watumie matini, hadithi, picha na chati zinazoonesha maumbo ya nahau na maana zake katika ufundishaji na ujifunzaji ili wanafunzi wawe mahiri katika kutumia nahau mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

(d) Walimu wawapatie wanafunzi mazoezi ya kutosha kwa kutumia matini au chati zinazoonesha alama mbalimbali za uandishi kama vile, alama ya mshangao, kuuliza, kituo na mkato katika sentensi au habari fupi ili kuwawezesha wanafunzi kuzitumia alama hizo kwa ufasaha katika mawasiliano yao ya kila siku.

(e) Walimu wahakikishe kwamba wanafunzi wanapewa vifungu vya habari/hadithi, yakiwemo maelekezo ya kusoma na kujibu maswali watakayoulizwa, ili kuwajengea umahiri wa kusoma, kuelewa na kuutumia msamiati mpya katika mazingira mbalimbali.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## ULINGANIFU WA UFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2021 NA SFNA 2022

| Na. | Umahiri Mkuu | Upimaji 2021 | | | | Upimaji 2022 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya Swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 84.0 | 61.66 | Wastani | 1 | 82.10 | 51.84 | Wastani |
| | | 2 | 59.2 | | | 4 | 35.34 | | |
| | | 3 | 41.8 | | | 3 | 38.08 | | |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 5 | 74.8 | 54.05 | Wastani | 5 | 63.20 | 55.38 | Wastani |
| | | 4 | 33.3 | | | 2 | 47.56 | | |